# OFISI YA RAIS
# TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
# HALMASHAURI YA JIJI YA DAR ES SALAAM
# SHULE YA SEKONDARI MVUTI

**Anwani ya simu**
**Simu: +255 765 421313**
**OFISI YA MKUU WA SHULE.**
**KATA YA MSONGOLA.**

**S.L.P 69032.**
**DAR ES SALAAM,**
**TANZANIA**

Kumb. Na. MVT/SEK/F1/2024
JINA LA MWANAFUNZI
……………………………………………………
S.L.P ………………………………………………………
……………………………………………………………

**YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI MVUTI HALMASHAURI YA JIJI YA DAR ES SALAAM MKOA WA DAR ES SALAAM MWAKA 2024.**

**1.0 Utangulizi**

Ninafurahi kukuarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na kidato cha **KWANZA** kama mwanafunzi katika shule hii kwa mwaka 2024. Shule ya Sekondari **MVUTI** ipo kusini mwa Jiji la Dar es salaam.

Muhula wa masomo unaanza tarehe 08.01.2024. Unatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe **05.01.2024** kwa ajili ya usajili.

**2.1 Mambo Muhimu ya Kuzingatia**

**2.2 Sare za Shule**

(a) **Wavulana** suruali 2 rangi ya Blue Bahari, Mashati 2 meupe, Soksi nyeusi jozi (pea) mbili (2), na viatu vyeusi vya kamba vyenye kisigino **Maelezo ya mshono** suruali ndefu mzunguko wa chini 16. Mashati ya mikono mifupi.

(b) **Wasichana** viatu vya ngozi vyenye kisigino kifupi na vya kamba (GIDAMU) jozi (pea)2, soksi nyeupe jozi 2, Sketi 2 rangi ya Blue Bahari, shati 2 Nyeupe mikono mifupi kwa wakristo au nusu Kanzu na majuba 2 meupe kwa waislamu.
**Maelezo ya mshono** Sketi ndefu inayogusa unyayo wa mguu. Mshono wa sketi ni Linda box.

(c) Sare ya michezo kwa shule hii ni Track Suit za blue kwa Wavulana, Track Suit za Zambarau kwa Wasichana na Raba nyeusi za michezo kwa wote.

**2.3** Daftari (Counter book) 10, daftari za kawaida za mazoezi (msomi) 10 Kalamu na Mkebe wa Hesabu na vifaa vyake, na faili ajili ya kutunzia kumbukumbu za kitaaluma hapa shuleni.

**2.4** **Kwa wanafunzi wa kutwa**; Chakula cha mchana, nauli ya kwenda shuleni na kurudi nyumbani pamoja na matibabu ni jukumu la Mzazi/ mlezi.

**2.5** **Kwa wanafunzi wa bweni;** Nauli ya kwenda shuleni na kurudi nyumbani

wakati wa likizo, Godoro, Vifaa vya Malazi ni Jukumu la Mzazi/Mlezi. Ni wajibu wa mzazi kuhakikisha kwamba kila mwanafunzi anakuwa na kadi ya bima ya afya kwa ajili ya matibabu.

**2.6** **Vifaa vya usafi kwa wanafunzi wote wa kutwa na bweni;** ni wajibu wa mzazi/mlezi kuhakikisha kwamba mwanafunzi anakuja na ufagio mrefu wa chelewa wenye mpini wa kufagilia uwanja pamoja na kwanja (kwanja/panga/jembe) moja kwa ajili ya kufyekea vichaka na majani yanayozunguka eneo la shule.

***3.1*** **Sheria na Kanuni Muhimu za Shule.**

*3.2* Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia, yenye dhamana ya elimu nchini na ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na Uendeshaji Elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake baada ya kuripoti shuleni.

a. Heshima kwa viongozi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
b. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima.
c. Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni (Preparation) kwa wakati.
d. Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa.
e. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
f. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule
g. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa.
h. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.
i. Kutunza mali za umma.

***3.3*** **Makosa yafuatayo yanaweza kusababisha kufukuzwa au kusimamishwa shule.**

i. Wizi.
ii. Uasherati na ushoga.
iii. Ubakaji.
iv. Ulevi, uvutaji sigara na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi, cocaine, mirungi, kubeli na kadhalika.
v. Kupigana au kupiga.
vi. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.
vii. Kudharau Bendera ya Taifa.
viii. Kuoa au kuolewa kutoa mimba.
ix. Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.
x. Kukataa adhabu kwa makusudi.

xi. Kuwa na simu ya mkononi.

**4.1 Mambo mengine muhimu yanayopaswa kukamilishwa na kuwasilishwa shuleni na mwanafunzi.**

a) Medical examination form ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali. Fomu hii itakabidhiwa kwa Mkuu wa Shule mara utakaporipoti shuleni.

b) Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria ya elimu namba 25 ya mwaka 1978 na kufanyiwa marejeo mwaka 2015.

c) Picha mbili (passport size) za wazazi/ walezi ( baba moja, mama moja)

d) Picha mbili (passport size ) za mwanafunzi.

**5.1** Tafadhali soma kwa makini maelezo/ maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**KARIBU SANA**

**..........................................**

**GASPER A. MWAIPOPO**

**MKUUWASHULE**

**MVUTI SEKONDARI**

**KIAMBATANISHO A**

**MINISTRY OF EDUCATION, SCIENCE AND TECHNOLOGY**
**MVUTI SECONDARY SCHOOL**

PICHA YA MWANAFUNZI

To be completed by a Government Medical Officer

To Medical Officer

……………………………………..

Date ……………………………

**RE:** ……………………………………………………………………………………..

Please examine the person mentioned above and comment on his/her health responsible to the following items. Kindly put a tick or cross in front of either YES or NO

Does the student has problems in connection with

a) Sight?..........................................................................................................1. NO
2.YES
If yes, state.......................................................................................
b) Hearing ..........................................................................................................1.NO
2. YES
If yes, state.......................................................................................
c) Speech ..........................................................................................................1. NO
2. YES
If yes, state.......................................................................................
d) T.b?..........................................................................................................1.NO
2. YES
If yes, state.......................................................................................
c) Blood pressure..........................................................................................................1. NO
2. YES
If yes, state.......................................................................................

d) Any physical disability................................................................................ 1. NO
2.YES
If yes, state.......................................................................................
e) Do you therefore, recommend the said student medically: in for studentship at this section?
I. Yes 2. No
If no please state...............................................................................................

Date …………………………….. Name & Signature ………………………………...

Designation's stamp …………………………………………………

## KIAMBATANISHO KWA WANAFUNZI WA HOSTEL

Uongozi wa shule unayofuraha kukutaarifu kwamba mwanao amepangiwa kukaa Hostel. Mzazi utawajibika kutimiza wajibu wako kuzingatia maelekezo ya kujiunga na shule ya sekondari MVUTI, hii ni pamoja na matibabu ya mwanao, nauli ya kwenda nyumbani na kurudi shuleni wakati wa likizo, vifaa vyake vya kutumia awapo Hostel.

**MASHARTI:**

Uhitaji wa Hostel ni mkubwa hivyo mwanao hataendelea kuishi Hostel ifikapo mwisho wa mwaka endapo atashindwa kutimiza masharti ya Hostel na si mtoto tu hata wewe mzazi unaweza kusababisha mwanao asiendelee kuwepo hostel na kuwapisha watoto wengine ambao wanauhitaji huo.

1. Atawajibika kupata ufaulu wa daraja la **KWANZA** hadi la **TATU** ifikapo mwisho wa mwaka wa masomo. Wastani huu ni majumuisho ya mitihani na majaribio yote ya mwaka husika.
2. Mawasiliano yote kati ya mzazi/mlezi na mwanafunzi yatafanyika kupitia kwa Mkuu wa Shule/ Makamu Mkuu wa Shule au mwalimu mlezi wa hostel.
3. Mzazi atawajibika kuacha mawasiliano ya simu ambayo itapatikana muda wote na hataruhusiwa kufika shuleni kuonana na mtoto isipokuwa siku maalum ya kumtembelea mwanafunzi itapangwa na uongozi wa shule na taarifa zitawafikia wazazi na walezi.
4. Mtoto atawajibika kufuata masharti na taratibu zote atakazopewa awapo Hostel.
5. Kila mzazi ni lazima ahakikishe kuwa mtoto amekatiwa **BIMA YA AFYA** kwa ajili ya matibabu.

**VIFAA VYA HOSTEL KWA WASICHANA**

(1) Sahani, bakuli, kikombe (rangi ya bluu) viwe vya plastiki ya mfupa na kijiko

(2) Ndoo (lita 10) na beseni kwa ajili ya kuogea na kufulia

(3) Taulo, shuka mbili rangi ya PINKI, mto (pillow) yenye foronya ya PINKI, Chandarua, tandiko la futi tatu (3) Pasi ya mkaa

(4) Shamba dress (KITAMBAA ULICHOPEWA)

(5) Ufagio (soft broom), Mopa na ndoo yake na ufagio wa chooni (hard broom).

**VIFAA VYA HOSTEL KWA WAVULANA**

(1) Sahani, bakuli, kikombe (rangi ya bluu) viwe vya plastiki ya mfupa na kijiko

(2) Ndoo (lita 10) na beseni kwa ajili ya kuogea na kufulia

(3) Taulo, shuka mbili rangi ya BLUE, mto (pillow) yenye foronya ya BLUE, Chandarua, tandiko la futi tatu (3) Pasi ya mkaa.

(4) Shamba dress (KITAMBAA ULICHOPEWA)

(5) Ufagio (soft broom), Mopa na ndoo yake na ufagio wa chooni (hard broom).

**MAKOSA YANAYOWEZA KUMUONDOA MWANAFUNZI HOSTEL**

1. Kuvunja sheria za shule.
2. Uchafu wa mwili, nguo, na vyombo anavyotumia.
3. Kuvaa nguo zisizo ruhusiwa kwa wakati unaotakiwa au kuvaa mavazi ambayo hayafuati maadili (nguo fupi na zinazobana au kaptura)
4. Kushindwa kuhudhuria masomo/ maandalizi ya masomo usiku kwa muda unaotakiwa na kusumbua wenzie kwa kupiga makelele au kulala badala ya kusoma.

5. Kushindwa kuungana na wenzie katika swala au maombi kabla ya masomo/ maandalizi ya masomo ya usiku wakati wa kuanza na wakati wa kwenda kulala.
6. Kuanzisha vikundi /magenge yasiyo na mwelekeo wa kimasomo.
7. Kuiba mali za wenzie bwenini.
8. Kusingizia kuumwa kusudi apate fursa ya kutokufanya mitihani au kurudi nyumbani.
9. Kushindwa kupata wastani wa alama za masomo unaokubalika kwa mwanafunzi wa hostel.
10. Mzazi kutokuhudhuria vikao viwili mfululizo vya wazazi wenye watoto hostel na vya shule kwa ujumla.

Mwisho mzazi unatakiwa kukiri kwamba unakubali masharti na taratibu hizi zote na upo tayari kukubali mwanao kuondolewa Hostel endapo masharti yamekiukwa na wewe mwenyewe au mtoto kama ilivyo elekezwa.

Pia unatakiwa kuhudhuria vikao vyote vya shule na vya wazazi wenye watoto Hostel. Hivyo kusaini kwako hapa inachukuliwa kwamba umekubaliana na sheria /taratibu zote za mwanao kukaa hostel.

**TAMKO LA MZAZI/MLEZI**

| |
|---|
| **PICHA YA MZAZI/MLEZI** |

Mimi mzazi/mlezi wa (Jina la Mtoto) ................................ ...........................nakiri kwambanimesoma na kuzielewa kanuni/ taratibu na sheria za shule kwa ajili ya mwanangu awapo hostel/shuleni, hivyo nitakuwa tayari kukubaliana na maamuzi yoyote yatakayo chukuliwa na uongozi wa shule endapo mwanangu atakiuka kanuni/ taratibu na sheria zilizo ainishwa hapo juu.

Jina la Mzazi ………………………………………………………………………………

Sahihi ya Mzazi ……………………………………………………..………………

Na. Simu (Mzazi /Mlezi) ……………………………………………………………

Tafadhali jaza sehemu hii hapa chini kukiri kwamba umesoma na kuelewa maelezo ya fomu hii.
Hivyo kusaini kwako hapa inachukuliwa kwamba umekubaliana na sheria /taratibu zote za mwanao kuwepo hapa shuleni.